**JAMHURIYA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA UZINDUZI WA KITUO CHA MABASI NA MAEGESHO YA MALORI NYAMHONGOLO, ILEMELA, MWANZA,

**13 SEPTEMBA 2022.**

- ***Mheshimiwa Innocent Bashungwa (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI;***
- ***Mawaziri, Manaibu Waziri na Wabunge wote mliopo;***
- ***Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza;***
- ***Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Mwanza;***
- ***Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa;***
- ***Ndugu Balandya Mayuganga, Katibu Tawala wa Mkoa;***
- ***Mheshimiwa Renatus Mulunga, Mstahiki Meya wa Jiji La Mwanza;***
- ***Viongozi wetu wa Dini;***
- ***Ndugu Waandishi wa Habari;***
- ***Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…***

***Mwanza oyee…***

***Rais Samia Suluhu Hassan oyee…***

Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema, kwa kutupa uhai na kutuwezesha kukutana hapa leo. Naomba nitumie fursa hii kuwapongeza sana wana Mwanza na wana Ilemela kwa kupata Kituo hiki kizuri cha Mabasi na Maegesho ya Malori. Vilevile, niwapongeze Kampuni iliyojenga ya STECOL Corporation ya nchini China; Kamati ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi kwa ufuatiliaji wa karibu; na wote waliosimamia ujenzi wa Kituo hiki toka kuanza kwake Julai 2019 hadi leo ninapokizindua rasmi.

Kipekee kabisa napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Wananchi wa Mkoa wa Mwanza kwa kuendelea kufanya kazi kwa bidii katika sekta mbalimbali hususan za kilimo, ufugaji na uvuvi ili kujiletea maendeleo. Mchango wenu katika pato la Taifa ni mkubwa na tunauthamini sana. Hongereni sana kwa kufanya kazi kwa bidii na endeleeni na uchapakazi huo kwani hata vitabu vya dini vinaeleza kuwa tufanye kazi kwa bidii na asiyefanya kazi asile.

Vilevile, napenda kuupongeza uongozi na wananchi wa mkoa wa Mwanza kwa kuratibu na kukamilisha zoezi la Anuani za Makazi ambalo limekamilika kwa asilimia 100 na Zoezi la Sensa ya Watu na Makazi kwa ufanisi mkubwa. Kwa taarifa za awali kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu (NBS), zoezi la Sensa ya Watu na Makazi limefanyika kwa ufanisi. Hongereni sana wananchi wa Mwanza kwa

kuhamasika na kujitokeza kushiriki kikamilifu katika mazoezi yote mawili kwa maendeleo ya nchi yetu.

***Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana***

Nafahamu namna ambavyo, kukamilika kwa mradi huu wa kimkakati kumeondoa kero ya muda mrefu iliyokuwa inawakabili wananchi wa Jiji la Mwanza. Kero hizo ni pamoja na msongamano wa magari na watu kwenye kituo cha zamani cha mabasi cha Buzuruga pamoja na maegesho holela ya malori. Vilevile, kama tulivyoelezwa, mradi huu uliosheheni huduma mbalimbali kama Maduka, Migahawa, Benki, Nyumba ya kulala wageni nk., unatoa fursa kwa wananchi wa Jiji letu hili la Mwanza kufanya biashara kwenye Kituo hiki kupitia maeneo yaliyopangwa kwa ajili ya biashara. Hivyo, ninawaomba wananchi kuchangamkia fursa hizo za biashara pamoja na fursa mbalimbali za ajira zilizopo kutokana na Kituo hiki.

***Waheshimiwa Viongozi, Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana***

Katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2020-2025 na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ametoa fedha zaidi ya shilingi bilioni 25 kuhakikisha Kituo hiki cha kisasa kinakamilika. Nia njema ya Mheshimiwa Rais ni kuona wana Mwanza na wana Ilemela wanafanya biashara zitakazowasaidia kupata vipato na kuhudumia familia zao na pia kulipa kodi zitakazotumika katika miradi mingine ya maendeleo.

Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea kutoa kipaumbele kwa kuimarisha miundombinu ya usafirishaji katika Mkoa wa Mwanza na Kanda ya Ziwa kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali. Miradi hii ni pamoja na; Upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Mwanza likiwamo jengo la kisasa la abiria; Ujenzi wa Meli ya MV-Mwanza ambao umefikia asilimia 71 na meli hiyo inatarajiwa kuingia kwenye maji Oktoba 2022; na Ujenzi wa daraja la Kigongo – Busisi ambao unaendelea vizuri na unatarajiwa kukamilika ifikapo Februari 2024. Hali kadharika, ujenzi wa reli ya kisasa kipande cha Isaka-Mwanza unaendelea. Naamini kukamilika kwa miradi hii kutaipaisha Mwanza na Kanda ya Ziwa kuwa miongoni mwa kitovu kikubwa cha biashara katika Ukanda wa Afrika Mashariki.

Pamoja na utekelezaji wa miradi hii, Serikali imeleta pia fedha nyingi hapa Mkoa wa Mwanza kwa ajili ya miradi mingine mingi ya maendeleo. Na Serikali imefanya hivi kwa nchi nzima. Ninawataka watendaji wote wasimamie fedha hizo na kuhakikisha zinatumika kama ilivyokusudiwa na thamani ya fedha

inapatikana. Halmashauri zote wekeni nguvu katika kukusanya mapato ya ndani na kuhakikisha fedha hizo zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

***Waheshimiwa Viongozi, Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana***

Nafahamu mara kadhaa kwenye vituo kama hivi kunakuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kwa ajili ya kupata vizimba vya kufanyia biashara zao. Hivyo, nauagiza Uongozi wa Mkoa kutoa vizimba vya biashara vilivyotengwa kwenye Kituo hiki bila upendeleo. Kuna tabia kwa baadhi ya viongozi kwa kutumia nyadhifa zao kushikilia maeneo mengi na walengwa kukosa ama kuwekewa vikwazo kupata vizimba. Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, hakikisheni kunakuwa na uwazi katika utaratibu utakaotumika kutoa vizimba hivi. Na, kwa kuwa mimi ndio nimefungua rasmi Kituo hiki, nitafuatilia na kuhakikisha hakuna upendeleo katika ugawaji wa vizimba vya biashara na kwamba, utaratibu uwe jumuishi ukizingatia makundi maalumu kama wenye ulemavu, vijana na wanawake.

Aidha, tunzeni miundombinu ya Kituo, ikiwa ni pamoja na mifumo ya maji, umeme, na vyoo. Pia, hakikisheni uwepo wa huduma madhubuti za kukabiliana na majanga kama moto; huduma ya kwanza pamoja na utaratibu mzuri wa ukusanyaji wa taka ikiwamo vifaa na teknolojia zinazofaa katika kukusanya na udhibiti wa taka. Aidha, wekeni ulinzi imara kuzunguka eneo hili ili kuimarisha usalama wa watu na mali zao hususan wageni na wasafiri wanaotumia kituo hiki.

***Waheshimiwa Viongozi, Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana***

Katika baadhi ya vituo kama hivi katika mikoa yetu bado hawajaweka utaratibu mzuri wa ukusanyaji wa mapato. Hivyo, ninyi muwe mfano mzuri na wa kuigwa katika ukusanyaji wa mapato katika kituo hiki. Hakikisheni mnasimamia na kuweka mifumo bora ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato yanayotokana na uendeshaji wa Kituo hiki. Sitaki kuja kusikia mapato yameaanza kupotea katika kituo hiki. Mianya yote ya upotevu wa mapato izibwe kabisa na wale ambao wanategemea kujinufaisha na mapato ya Kituo hiki dawa yao inachemka, hatutowavumilia kabisa. Tambueni kuwa fedha hizi zilizotumika kukamilisha huu mradi ni za wananchi hawa wanyonge, hivyo sitegemei kusikia mapato yatakayokusanywa hapa yanaishia mifukoni mwa watu. Nataka kuona mabadiliko katika mapato ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kufuatia ujenzi wa Kituo hiki. Nilipokuwa napitia ripoti ya Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Ilemela, nikaona mmekusanya shilingi bilioni 2.8 tu katika kipindi cha mwezi Aprili-Juni 2022. Sasa tunatarajia makusanyo yenu yataongezeka maradufu mkisimamia vizuri Kituo hiki.

Vilevile, nawaagiza pia Uongozi wa Mkoa na Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kuondoa kero ya vumbi na tope nilizoziona jirani na Kituo hiki. Nimeelezwa kuwa vumbi hilo linasababishwa na kituo cha daladala kilicho jirani na Kituo hiki. Naamini hili liko ndani ya uwezo wenu. Pamoja na hatua nyingine, hakikisheni mnapanda miti ambayo itasaidia kupunguza vumbi, kuleta kivuli na maua kwa ajili ya kupendezesha mazingira. Natumie fursa hii pia kuelekeza suala hili la upandaji wa miti na upendezeshaji wa Vituo vya Mabasi litekelezwe nchi nzima. Nimehudhunishwa sana na Manispaa ya Jiji la Dar es Salaam ambapo hadi sasa bado hawajapanda miti ya kutosha kunzunguka Kituo cha Mabasi cha Magufuli. Uzembe huo hauvumiliki kwani mchoro wa Kituo hicho unaonesha bayana maeneo ya kupanda miti na maua.

***Waheshimiwa Viongozi, Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana***

Katika kuhitimisha hotuba yangu napenda kusisitiza na kuelekeza mambo machache yafuatayo:

***Jambo la Kwanza***; Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Uongozi wa Mkoa wa Mwanza, mhakikishe kuwa Kituo hiki kina huduma za majokofu (cold rooms) kwa ajili ya kuhifadhia shehena ya bidhaa zinazoharibika katika kipindi cha muda mfupi kama samaki, matunda na mbogamboga. Vilevile, huduma hizo zitaongeza mapato yenu.

***Jambo la Pili***; Nafahamu mna mpango wa kujenga jengo la Wamachinga pembeni mwa Kituo hiki. Anzeni mara moja, mradi huo unalipa na utasaidia kutengeneza ajira na kipato cha mtu mmojammoja na Manispaa hii kwa ujumla. Katika Ilani ya CCM katika ibara yake ya 24 (a) inasisitizwa kutengwa kwa maeneo kwa ajili ya wajasiriamali wakiwamo mama lishe, wauza mboga na wanyabiashara wadogo ili kuyawezesha makundi hayo kufanya shughuli zao bila bugudha. Angalizo langu katika eneo hili ni kwamba, hakikisheni ujenzi wa jengo hilo la Wamachinga unazingatia sheria za mipango miji ili usiathiri shughuli za Kituo hiki na mtiririko wa mabasi na malori yanayoingia na kutoka katika eneo hili.

***Jambo la Tatu***, Uongozi wa Mikoa na Halmashauri katika Ukanda huu wa Ziwa msibweteke mnatakiwa kuwa wabunifu wa kuwa na shughuli ambazo zitachochea ukuaji wa uchumi. Ili mnufaike na kuona faida ya kuwa na Vituo kama hivi lazima mchochee ukuaji wa shughuli zingine za kiuchumi. Fursa katika Ukanda huu ni nyingi. Hata hivyo, viashiria muhimu vya uchumi katika Ukanda huu haviridhishi. Msikubali muendelee kuwa na kiwango kikubwa cha umasikini licha ya rasilimali lukuki mlizojaaliwa na Mungu. Nawataka pia

muongeze ubunifu na kupanua wigo wa shughuli zenu za kuichumi, kwa mfano:

(i) Bado hamfanyi vizuri katika utalii hususan kuwekeza katika vivutio vya utalii katika Ziwa Victoria ili mnufaike zaidi na uwepo wa mtandao mzuri wa huduma za usafirishaji na vivutio vingine vya utalii kama mbuga ya wanyama maarufu duniani ya Serengeti ambayo ipo karibu sana na mkoa huu;

(ii) Ongezeni wigo wa mazao (crop diversification) ikiwamo kilimo cha bustani za matunda na mbogamboga. Elekezeni sehemu ya mapato yenu ya ndani kujenga miundombinu ya umwagiliaji. Igeni mikoa ya Kaskazini na Nyanda za Juu Kusini ambayo imefanikiwa sana kupitia kilimo cha umwagiliaji hata kuongeza Pato la Mtu mmojammoja kuwa takribani shilingi milioni 4 kwa mwaka, ikichuana na Dar es Salaam; na

(iii) Vutieni viwanda vya kuchakata maziwa, ngozi na bidhaa zake. Bado hamfanyi vizuri katika eneo la viwanda licha ya kuwa na malighafi za kutosha. Fikirini nje ya boksi kwa kuongeza wigo wa viwanda zaidi ya hivi vichache vilivyopo sasa vya chuma na vinywaji.

***Jambo la Nne***, Mikopo nafuu kwa makundi maalumu itokanayo na asilimia 10 ya mapato yenu ni nguzo muhimu katika kuyawezesha makundi hayo kushindana na wengine katika Kituo hiki. Hata hivyo, taarifa nilizonazo fedha hizo haziendi kwa walengwa na mnakabiliwa na mabilioni ya mikopo chechefu. Nauagiza Uongozi wa Mkoa kutafuta muarobaini wa dosari hiyo inayochafua rekodi nzuri ya Mkoa huu. Hakikisheni sheria na taratibu za mikopo hiyo zinafuatwa.

***Jambo la Tano***, napenda kutumia fursa hii kukemea mimba na ndoa za utotoni. Mimba na ndoa za utotoni hazikubaliki kwa sababu: ni kinyume na sheria na maadili yetu; zinawanyima fursa watoto wetu wa kike kusoma na kufikia malengo yao; zinapelekea vifo na matatizo ya fistula kwa watoto wetu wa kike; na ni ukatili dhidi ya watoto wetu wa kike. Hili halikubaliki. Nautaka uongozi wa mkoa wa Mwanza kuhakikisha watoto wetu wanasoma na kumaliza masomo. Hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi ya wote watakaobainika na kuhusika kuoa ama kuozesha watoto na wale watakaobainika kusababisha watoto wetu wa kike kupata mimba za utotoni. Waacheni watoto wetu wa kike wasome msiwakatishe malengo yao.

***Jambo la Sita,*** ni utitiri wa vituo vya mafuta kwenye makazi ya watu na vingi kujengwa karibu karibu. Wanaohusika na utoaji wa vibali wazingatie sheria na taratibu ili baadaye visije kuleta madhara kwa Wananchi.

***Waheshimiwa Viongozi, Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana***

Napeda nimalizie hotuba yangu kwa kuwapongeza Wabunge wote wa Mkoa wa Mwanza kwa ushirikiano wenu katika kutetea maslahi ya wananchi wenu. Nawasihi muendelee kuhakikisha Serikali inawajibika na kutekeleza ahadi zake kwa wananchi.

Mwisho kabisa, nawashukuru wananchi wote kwa kufika kwa wingi kwenye ufunguzi rasmi wa Kituo hiki cha Mabasi na maegesho ya malori na napenda niwaahidi kuwa nitarudi tena kufanya ziara rasmi katika mkoa huu. Niwakumbushe tena, zitumieni fursa katika Kituo hiki kikamilifu.

Baada ya kusema hayo, natamka kwamba Kituo cha Mabasi na Maegesho ya Malori Nyamhongolo Wilaya ya Ilemela sasa nimekizindua rasmi.

**MWANZA OYEE!**

**MUNGU AWABARIKI SANA.**

**AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA!**